TANGAZO LA SERIKALI NA. 769 tarehe 30/12/2022

SHERIA YA MISITU,
(SURA YA 323)

# NOTISI

(*Imetengenezwa chini ya kifungu cha 23(1))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA MSITU WA KARUWE KUWA MSITU WA HIFADHI WA KARUWE YA MWAKA 2022

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Msitu wa Karuwe Kuwa Msitu wa Hifadhi wa Karuwe ya Mwaka 2022.

Eneo linalopendekezwa kutangazwa

2. Eneo la msitu ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Notisi hii linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Karuwe.

Madhumuni ya tangazo

3. Madhumuni ya kupendekezwa kutangaza Msitu wa Karuwe kuwa Msitu wa Hifadhi wa Karuwe ni-

(a) kulinda eneo lililohatarini la Msitu wa Hifadhi wa Karuwe ambalo linatambulika kwa thamani yake ya juu ya baioanuwai, lenye upekee wa mimea na wanyama, ikijumuisha spishi za mimea na wanyama waliohatarini, baadhi yao wako katika hatari ya kutoweka; na

(b) kuhifadhi, kuendeleza, kusimamia na kutumia kwa uangalifu rasilimali za misitu ndani ya Eneo la Msitu wa Hifadhi Karuwe ili kuongeza mchango wa sekta ya misitu katika maendeleo endelevu ya Tanzania.

Uhalali wa Notisi

4. Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa na ndani ya

kipindi hicho mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza kwa maandishi-

(a) kupinga;
(b) kuwasilisha maoni; au
(c) kudai haki zozote zinazotokana na sheria za kimila,

kuhusiana na ardhi au mazao ya msitu au haki zozote zilizoainishwa kwenye sheria nyingine katika eneo ambalo linapendekezwa kutangazwa Msitu wa Hifadhi wa Karuwe.

Uwasilishaji wa mapingamizi

5. Mapingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya tangazo la Msitu wa Hifadhi wa Karuwe yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii kwa anauani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA.

*Tangazo la serikali na. 769 (linaendelea)*

---

**JEDWALI**

---

(*Limetengenezwa chini ya aya 2*)


WILAYA YA MBEYA

MSITU WA HIFADHI WA KARUWE

*Makadirio ya eneo:* Hekta 1225 au Kilometa za Mraba 12.25

Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la Msitu wa Karuwe sehemu ya Safu za Msitu wa Hifadhi wa Mbeya linalopatikana Wilaya ya Mbeya, Mkoa wa Mbeya kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 3093 ya Agosti 2021 (Skeli 1:20000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dodoma na lenye mipaka ifuatayo:




Dodoma
15 Desemba, 2022

PINDI H. CHANA,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*